

MRADI WA KUTENGENEZA MAANDAZI NA KUYASAMBAZA MADUKANI.

Mradi huu utahusisha utengenezaji wa vitafunwa aina ya maandazi na kuyasambaza maduka mbali mbali kwa ajili ya kununuliwa na wateja. Hivi ni vitafunwa vinavyojulikana na wengi mijini na vijijini. Vitafunwa hivi hutengenezwa na ngano inayouzwa madukani pamoja na mchanganvyiko wa viungo vingine mahsusi.

Ni mradi mdogo sana kwa kuutizama lakini kama ukifanywa kwa umakini unafaida kubwa na inaweza hata kumpatia mtengenezaji pesa nyingi. Ifutayo ni mchanganuo wa bajeti na mambo mengineyo ya jinsi ya kuifanya hii biashara kuwa na faida kubwa.

Usambazaji

Kama nilivyoainisha awali kuwa hii biashara itafanyika kwa kuweka maandazi haya madukani {maduka ya kawaida kwa kuwaomba marafiki na hata kuwa na makubaliano fulani}. Kwa mfano hapa mtengenezaji atakuwa na madeli {makontena} madogo kumi {10} ambayo kila moja wapo litakuwa na maandazi 100. Yote haya yata wekwa maduka tofauti tofauti kwa makubaliano Fulani Fulani na muuzaji. Hapa ujanja wa kuweka maandazi ma2 ama ma3 kwa kila deli ili kumpatia muuzani nae atafute kama ujira wake.

Utengenezaji

Maandazi yatatengenezwa na msambazaji mwenyewe kwa mikono yake ili kuepuka gharama kubwa za uwekezaji huu. Vifaa vitanunuliwa humu humu ndani ya nchi pia ili kuepuka gharama za uzalishaji na kujihakikishia faida kubwa.

Gharama za awali

Sn	Hitaji	Idadi ya hitaji	Gharama za hitaji
1.	Unga wa ngano {Chapa Azam}	Kg 50	100000
2.	Sukari	Kg 2	5000
3.	Viungo	Kg 1	5000
4.	Madeli	5 @ 5000	25000
5.	Amira	5000	5000
6.	Mafuta ya kupikia	Lita 20	50000
7.	Jiko la kupikia	1	50000
8.	Beseni kubwa la kukandia	2 @ 8000	16000
9.	Kijiko cha kugeuzia maandazi	1	5000
10.	Dhalula	-	50000
11.	Mkaa {kigunia kidogo}	1	20000
	Jumla ya gharama za awali		331,000

Mbinu za kuyafanya yauzike.

Kwa sababu huu ni ujasiriamali makini, sasa ili kuifanya hii bidhaa iuzike ni muhimu kuwa mbunifu. Nazani inaeleweka kuwa vipo aina nyingi ya vitafunwa madukani vizuri tuu lakini ni vema kuyafanya maandazi haya yakauzika mapema na haraka ili kuufanya mzunguko wa biashara uwe mzuri na wa haraka zaidi. Kwa mfano size ya andazi iwe ya kuridhisha kulingana na gharama za ununuzi wa bidhaa {kuepuka tamaa}, kuweka viungo ili angalau andazi liwe na harufu na radha ya kuvutia, kuweka tui la nazi, maandazi yakae

katika hali ya usafi yaani yaka ndani ya deli linalo yaonesha {transparent} lililofunikwa na pia ili kuepuka mandazi yasiwe na unyevu nyevu ni vema deli likatobolewa matundu kiasi ili kupitisha hewa.

Changamoto.

Bithaa hii ikiwa sokoni itakutana na bidhaa nyingine kama hizi, kwa hiyo ni vema ubunifu wa hali ya juu ukatumia ili kuifanya biashara hii kuwa ya kipekee na kupendwa na watu.

Mpango na idadi ya mauzo

Sn	Madeli	Maduka na idadi ya maandazi	Mauzo	Jumla ya pesa
1	Deli la kwanza	Duka 1 Maandazi 100	100×100	10,000
2	Deli la pili	Duka 2 Maandazi 100	100×100	10,000
3	Deli la tatu	Duka 3 Maandazi 100	100×100	10,000
4	Deli la nne	Duka 4 Maandazi 100	100×100	10,000
5	Deli la tano	Duka 5 Maandazi 100	100×100	10,000
6	Deli la sita	Duka 6 Maandazi 100	100×100	10,000
7	Deli la saba	Duka 7 Maandazi 100	100×100	10,000
8	Deli la nane	Duka 8 Maandazi 100	100×100	10,000
9	Deli la tisa	Duka 9 Maandazi 100	100×100	10,000
10	Deli la kumi	Duka 10 Maandazi 100	100×100	10,000
JUMLA YA MAUZO KWA SIKU				100,000

Mapato na Matumzi na Faida kwa mwezi na mwaka mzima wa biashara

	Kwa siku	Kwa mwezi {siku30}	Kwa Mwaka {Miezi 12}
Mapato	100,000	3,000,000	36,000,000
Matumizi	26,000	780,000	9,360,000
Faida	74,000	2,220,000	26,640,000

Yamkini kuna hesabu zimekosewa kwa njia moja ama nyingine lkn napenda kuwafungua macho watu waliokuwa wanaichukulia poa hii biashara, labda niwaambie mama yangu mzazi mimi kwa % Fulani kanilea mimi na ndugu zangu wengine kwa biashara ya maandazi. Sasa wewe mdau ni kazi yako wewe kusuka ama kunyoka. Ikumbukwe huu mradi unaweza kuufaya na vijana wako home hata kama unafanya kazi kwa {DEREVA WA ROLI} <≈ Usini-quote tafadhali

Prepared BY: Mkulima2002

JF Member

2017